MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA



# TIRA BULLETIN

Jarida Maalum kuhusu Mkutano wa kupokea Maoni na Malalamiko Kanda ya Kaskazini

## YALIYOMO

01 MKUTANO WA KUPOKEA MAONI NA MALALAMIKO KUHUSU BIMA KANDA YA KASKAZINI WAFANA Pg. 01

02 WATOA HUDUMA ZA BIMA WAASWA KUONGEZA UBUNIFU Pg. 02

03 NAIBU KAMISHNA WA BIMA ATOA UFAFANUZI KUHUSU BIMA YA TAKAFUL Pg. 03

04 KAMPUNI 23 ZAFUNGUA MATAWI KANDA YA KASKAZINI Pg. 04

05 MATUKIO KWA PICHA Pg. 05

Wahariri: Bi. Hadija Maulid na Bw. Zakaria Muyengi



# MKUTANO WA KUPOKEA MAONI NA MALALAMIKO KUHUSU BIMA KANDA YA KASKAZINI WAFANA

**Na. Hadja Maulid**

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania Kanda ya Kaskazini, imefanya mkutano uliowakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya bima wakiwemo watendaji wakuu wa kampuni za bima, mawakala, washauri wa bima, mabenki wakala wa bima, baadhi ya viongozi wa taasisi za Serikali na wananchi wanaotumia huduma mbalimbali za bima.

Mkutano huo uliofanyika tarehe 24 Agosti, 2023 katika ukumbi wa mikutano wa kimataifa jijini Arusha – AICC ulikuwa na mafanikio makubwa ambapo ulikusanya maoni, malalamiko na ushauri kutoka kwa wadau mbalimbali. Aidha jopo la wataalamu kutoka TIRA kwa kushirikiana na wataalam mbalimbali wa sekta ya Bima walitolea ufafanuzi, utatuzi na kuchukua hoja mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji.

Mkutano huo unafanya idadi ya mikutano ya aina hiyo kufikia Mitano ambapo mpaka sasa tayari imeshafanyika mikutano katika Kanda ya Ziwa Mwanza, Kanda ya Nyada za Juu Kusini-Mbeya, Kanda ya Kati-Dodoma, pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba Zanzibar.

Lengo la mikutano hii ni kupokea na kusikiliza pamoja na kutolea ufafanuzi maoni na malalamiko ya wananchi kuhusu huduma za bima nchini.



Aidha, Mamlaka itaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na wadau mbalimbali kwenye soko la bima ikiwa ni pamoja na kampuni zote za bima, mawakala wa bima na watoa huduma wengine wa bima pamoja na wananchi ambao ndio watumiaji wa bima. Mamlaka pia inaendelea kufanya kazi kwa karibu na washirika wake wengine kutoka taasisi mbalimbali za umma ikiwa ni pamoja na Wizara ya Fedha,Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Nishati, TRA, LATRA, TASAC, NIDA, NHIF na Jeshi la Polisi.

Ni kwa mantiki hiyo, Mamlaka inasisitiza kuendela kufanya mikutano hii muhimu sana kwa manufaa ya wananchi, watoa huduma za bima, na watumiaji wa bima nchini ili kulinda masilahi ya watumia bima,

kuendeleza soko la bima na hatimaye kuunga mkono harakati za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kukuza uchumi wa Taifa kupitia sekta yetu wa bima.

Wakati wa Mkutano huo, Kamishna wa Bima Dkt. Baghayo A. Saqware alitoa wito kwa watoa huduma za bima kufuata sheria, kanuni na taratibu za bima wakati wa kuwahudumia wananchi. Mkutano huo ulihudhuriwa na waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali vya habari. Aidha mkutano huo ulikuwa mbashara kupitia Youtube ya TIRA ambapo pia unaweza kupitia marudio yake hadi sasa.

#TIRA: Kwa Soko Salama la Bima




# WATOA HUDUMA ZA BIMA WAASWA KUONGEZA UBUNIFU

**Na. Hadja Maulid**

Watoa huduma za Bima nchini wameaswa kuongeza ubunifu katika kazi zao kwa kuongeza bidhaa mbalimbali za bima zinazozingatia uhitaji na zenye manufaa kwa watanzania hususani wananchi wa kipato cha chini kwani wananchi hao ni wengi na wanastahili kupata huduma mbalimbali za Bima.

Rai hiyo imetolewa na Kamishna wa Mamlaka ya Usimazi wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware mnamo Tarehe 24 Agosti 2023 kwenye Mkutano wa kupokea maoni na malalamiko kwa wananchi uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa AICC jijini Arusha. Kamishna amesema kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima, imeweka mazingira wezeshi kwa watoa huduma wote wa Bima kufanya kazi kwa ufanisi ili kuleta ustawi mzuri wa Soko la Bima Nchini.

"Mamlaka kwa upande mwingine tutaendelea kuboresha mazingira na usimamizi kwa ajili ya soko salama la bima nchini. Muhimu zaidi, tumieni nafasi mlizonazo kutoa elimu ya bima na nitoe rai kuwahamasisha watanzania wote kukata bima kama vile bima za maisha, bima za afya, bima za vyombo vya moto n.k ili kujikinga na majanga mbalimbali yanayoweza kutokea katika maisha na shughuli zetu za kila siku"

**Dkt. Baghayo Saqware.**

Kamishna pia amewahimiza wadau wa sekta ya bima kutumia fursa zilizopo kupitia Miongozo mbalimbali iliyotolewa na Mamlaka. Ni kwa mantiki hiyo, Mamlaka hivi karibuni imeweza kutoa Miongozo mbalimbali ambayo ni; Miongozo ya Usimamizi wa Ubakizaji wa Bima na Bima Mtawanyo, Miongozo ya Bima ya Afya na Usajili wa Watoa Huduma za Afya, na Miongozo ya Utoaji Ithibati kwa Warekebishaji na Watengenezaji wa vyombo vya Moto wanao wahudumia sekta ya bima. Aidha miongozo mingine iliyopo ni Mwongozo wa Uendeshaji huduma za Takaful; Mwongozo wa Utoaji Huduma za Bima Kidijitali; Mwongozo wa Maafisa Wauza Bima; Mwongozo wa Utekelezaji wa viwango vya kimataifa vya taarifa ya kifedha kuhusu mikataba ya bima (IFRS 17);Mwongozo wa Uwekezaji na Usimamizi wa Ukwasi; Mwongozo wa Kushughulikia Madai ya Bima; Mwongozo wa Uendeshaji wa Biasharaya Benkiwakala; Mwongozo wa Viwango Elekezi vya Fidia ya Bima kwa Madai ya Majeraha ya Mwili na Vifo kwa mtu wa tatu kutokana na ajali za magari. Miongozo hii ina lengo la kusimamia, kukuza na kuendeleza sekta ya bima.




# NAIBU KAMISHNA WA BIMA ATOA UFAFANUZI KUHUSU BIMA YA TAKAFUL

**Na. Pastory Mabonesho**

Naibu Kamishna wa Bima Bi. Khadija Said ametoa ufafanuzi kuhusu Bima ya Takaful ambapo baadhi ya Wadau walioshiriki kwenye Mkutano wa kupokea maoni na malalamiko ya bima Kanda ya Kaskazini walitaka kujua kuhusu bima hiyo.

Naibu Kamishna amesema kuwa Takaful ni mfumo wa bima ambao unajumuisha vipengele vya kuchangiana na kushirikiana bila kujali imani na mafungamano ya mtu. Ni mfumo wa bima ambao washiriki hutoa sehemu au michango yao yote chini ya usimamizi wa Muendeshaji ambaye kazi yake ni kusimamia shughuli za uendeshaji, kulipa fidia na kuwekeza kwa misingi ya Shariah za Kiislamu.

Akiendelea kufafanua wakati wa mahojiano maalum, Naibu Kamishna Bi. Khadija Said amesemaTakaful imejengwa juu ya misingi miwili ambayo ni Mfumo wa Ushirika ambapo ni kundi ambalo limeunda mfuko jumuishi wa kukabiliana na majanga kwa kushirikiana. Mfuko jumuishi unamilikiwa na wanachama au washiriki wote. Msingi mwingine unajulikana kama Tabarru ambayo michango au msaada inayotolewa na washiriki wa Mfuko wa Takaful kwa ajili ya kuwafidia waathirika wa majanga pale yanapotokea.

Naibu Kamishna amemaliza kwa kusema kuwa muendesha wa biashara ya Takaful anawajibika kuendesha shughuli hizo katika misingi ya Shariah na kwa ajili ya maslahi ya washiriki. Hii ni pamoja na kuendesha biashara akizingatia misingi ya shariah na weledi. Amesema maelezo yote kuhusu Bima hii yamo kwenye Mwongozo wa uwendeshaji wa Takaful wa mwaka 2022.








# KAMPUNI 23 ZAFUNGUA MATAWI KANDA YA KASKAZINI

**Na. Hadja Maulid**

Kampuni 23 zinazotoa huduma ya bima nchini zimefungua matawi Kanda ya Kaskazini ikiwa ni sawa na asilimia 70% ya kampuni zote nchini. Hayo yameelezwa na Bi. Gladness Lema Meneja wa Kanda ya Kaskazini wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)

Bi. Gladness ameeleza kuwa matawi hayo yote yana ofisi katika Mkoa wa Arusha.
Aidha ametoa rai kwa kampuni za bima ambazo hazijafungua matawi au ofisi zake katika Kanda ya Kaskazini kuchangamkia fursa na kusogeza huduma za bima kwa wananchi kwani kanda ya Kaskazini ni sehemu yenye uhitaji mkubwa wa huduma za bima ikiwa hasa kwenye maeneo ya madini, utalii, ufugaji, kilimo, wafanyabiashara wadogo na wa kati.

Kuhusu Washauri na madalali wa bima, Meneja Gladness alisema kati ya kampuni 114 za bima zilizosajiliwa nchini, kampuni nane zipo kanda ya Kaskazini, sawa na asilimia Saba ya kampuni zote, ambapo kampuni Sita zipo Arusha, na kampuni mbili Kilimanjaro.

Kwa upande wa matawi ya mauzo Meneja Gladness alisema kati ya kampuni 114,
Matawi ya mauzo katika Kanda ya Kaskazini yapo 11 sawa na asilimia 9.6 matawi 10 yakiwa katika Mkoa wa Arusha na tawi Moja likiwa Mkoa wa Kilimanjaro. Aidha Kanda imesajili benki wakala mmoja.



"Mwaka 2022 tulikuwa na washauri bima Saba na mwaka 2023 wamefikia Wanane na hatujamaliza mwaka, hivyo ni mategemeo yetu, kutokana na juhudi tunazoweka za kutoa elimu na kuonesha fursa zilizopo kwenye sekta ya bima wataendelea kuongezeka.." **Bi. Gladness.**

Kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka, Kanda ya Kaskazini ni miongoni mwa Kanda ambazo Sekta ya Bima inakuwa kwa kasi.










KUPOKEA NA
MALALAMIKO YA BIMA
KASKAZINI


2023





